# TNMC Habari

Toleo No. 0016

TOLEO MAALUMU Disemba, 2024

HALIUZWI www.tnmc.go.tz @tnmchabari



**Wauguzi,wakunga wahimizwa kuhuisha leseni**

Habari Uk. 06



**Prof. Janabi apendekezwa Kugombea Ukurugenzi WHO Afrika**

Habari Uk. 02

# Watahiniwa 5147 Wafanya Mtihani Wa Usajili Na Leseni



Habari Uk. 01

## Mhe. Mhagama: Kurejeshwa Kwa Toto Afya Kadi Kutaleta Matumaini Mapya

Habari Uk. 05

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania ni Mamlakaya Kisheria inayosimamia wanataaluma na taaluma za Uuguzi na Ukunga Tanzania chini ya Sheria ya Mwaka 2010 na kanuni zake (The Nursing and Midwifery Act, 2010) ili kuhakikisha huduma zinazotolewa na wauguzi na wakunga nchini Tanzania ni za kiwango kinachokubalika na salama kwa jamii.

# TIMU YA WAHARIRI

## MWENYEKITI

**Bi. Agnes Mtawa**

## MHARIRI

**Mwakapiso Ndimmyake**

## WARATIBU

**Irene Chilewa**
**Rose Mhando**

## MSANIFU JARIDA

**Ezekiel Nyalusi**

# Watahiniwa 5147 Wafanya Mtihani Wa Usajili Na Leseni



Na. Mwakapiso Ndimmyake

Jumla ya watahiniwa 5147 wauguzi na wakunga waliohitimu katika vyuo mbalimbali, wamefanya Mtihani wa usajili na leseni unaoratibiwa na Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) katika vituo vilivyotengwa kwenye mikoa sita ya Tanzania Bara.

Hilo limebainishwa na Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania, Bi. Agnes Mtawa, Mjini Kibaha mkoani Pwani, alipokutana na waandishi wa habari ambapo alibainisha vituo vya mtihani kuwa ni pamoja na Chuo Kikuu cha Dodoma ( UDOM) na Chuo kikuu cha Mtakatifu Yohana vilivyopo Jijini Dodoma, Chuo Kikuu cha Kampala- Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Ruaha (RUCU) Iringa, Tabora Polytechnic- Tabora, Chuo cha Tandabui Mwanza pamoja na Chuo cha IAA cha Jijini Arusha.

Msajili amesema mtihani huo utafanyika siku ya Ijumaa ya Disemba 20, 2024, ambapo kati ya watahiniwa 5147, wanajumuisha wahitimu ngazi ya Astashahada 86, Stashahada 4498, Shahada ya Uuguzi 537, Shahada ya Ukunga 11 na Shahada ya Uuguzi katika Utaoji dawa za usingizi na ganzi 15.

***"Aidha, mara hii kwa mara ya kwanza Baraza litatoa mtihani kwa wauguzi wataalamu wa utoaji dawa za usingizi na ganzi, ambapo mtihani huo umetanguliwa na mtihani wa vitendo kwa lengo la kupima, kuhakiki na kujiridhisha kama wanaumahiri wa kutosha katika kutoa huduma muhimu ya utoaji dawa za usingizi na ganzi kwa wagonjwa"*** Alisema Mtawa

Bi. Mtawa, pia amewataka watahiniwa wa Mtihani wa kada za Uuguzi na Ukunga, Kujiepusha na vitendo vya udanyanyifu wakati wa kufanya mtihani, kwani atakayebainika kufanya hivyo atakabiliwa na adhabu zilizoainishwa kwa mujibu Sheria.

***"Kila mtahiniwa ajiepushe na tabia za udanganyifu kabla ya Mtihani, akiwa katika chumba cha Mtihani na hata baada ya Mtihani, kwani ukibainika unajihusisha na udanganyifu wowote ni kosa kwa mujibu wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010 kifungu 19 (3) na kwa mujibu wa Sheria hii adhabu yake ni kufutiwa mtihani kwa mujibu wa kifungu 22 cha kanuni"***

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania TMNC ni mamlaka ya kisheria inayosimamia wanataaluma na taaluma za uuguzi na ukunga Tanzania, Chini ya Sheria ya Uuguzi na ukunga ya mwaka 2010 na kanuni zake (The Nursing and Midwifery Act 2010) ili kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa na wauguzi na wakunga nchini zinakiwango kinachokubalika na salama kwa jamii.

# Prof. Janabi apendekezwa Kugombea Ukurugenzi WHO Afrika



Na. Mwandishi Wetu

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Dkt. Samia Suluhu Hassan amempendekeza Prof. Mohamed Janabi (Mkurugenzi mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili) na mshauri wa Raisi kwa masuala ya afya kwa ajili ya kugombea nafasi ya Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika kufuatia kufariki dunia kwa Dkt. Faustine Ndungulile(Mb.) aliyekuwa Mkurugenzi Mteule wa Shirika hilo.

Dkt. Samia Suluhu Hassan ameyasema hayo Disemba 10, 2024 wakati akiwaapisha viongozi mbalimbali alio wateuwa hivi karibuni kwenye Ikulu Ndogo ya Tunguu Visiwani Zanzibar.

Kauli hiyo ya Rais Dkt. Samia inakuja siku chache kufuatia kifo cha aliyekuwa Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika Dkt. Faustine Ndugulile aliyefariki akiwa kwenye matibabu nchini India.

*"Tumeangalia CV nyingi tulizokuwa nazo, tumeona yako inafaa kupelekwa huko wakati utakapofika, hivyo tunaomba ujiandae,"* amesema Rais Dkt. Samia.

Shirika la Afya Duniani (World Health Organization - WHO ni kitengo cha Umoja wa Mataifa kinachoshughulikia masuala ya Afya kwa umma ikilenga kuunganisha juhudi za kitaifa za kupambana na magonjwa na kujenga Afya, Kati ya shughuli muhimu za WHO ni programu za kupambana na magonjwa yanayoathiri watu wengi kama vile Malaria, Ukimwi au SARS likiwa na nchi wanachama 193.



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA**
**BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA**

# Sisi tumehuisha Leseni zetu za kitaaluma.

**Wewe Je?** **kama Bado**

## UHUISHAJI WA LESENI ZA UUGUZI NA UKUNGA KWA MUHULA WA 2024-2027

Muuguzi na Mkunga unaelekezwa kuhuisha Leseni na kuhakikisha unakuwa na **CPD points** zinazohitajika, kama kigezo cha kuhuisha leseni yako inayokuruhusu kutoa huduma.

Aidha, unakumbushwa kuingia kwenye mfumo wa Baraza ***https://tnmcis.tnmc.go.tz/register*** ili kukamilisha taratibu za kuhuisha leseni.



@tnmchabari    website: www.tnmc.go.tz

# Wauguzi, Wakunga Nchini Watakiwa Kuendana na Teknolojia Mpya

Na. Mwandishi wetu

Wauguzi nchini wametakiwa kufanya kazi kulingana na mabadiliko ya teknolojia, kutokana na ubora wa vifaa vinavyowekwa katika hospitali nyingi hapa nchini ili kuwawezesha kutoa huduma iliyobora na ya haraka kwa wagonjwa.

Wito huo umetolewa na Kaimu katibu tawala Mkoa wa Singida, Bw. Romwald Mwendi, wakati akifungua kikao cha wauguzi wafawidhi na wasaidizi wao wa hospitali za rufaa za mikoa 28 ya Tanzania Bara, kwa niaba ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida.

***"katika miaka ya karibuni kumekuwa na mabadiliko ya tiba na mfumo hasa katika sayansi na teknolojia, hivyo ni bora wakajengewa uwezo juu ya mfumo mpya ili kuhakikisha wateja wanapata huduma bora inayoendana na wakatati."*** Alisema Bw. Mwendi



Naye Muuguzi Mkuu wa Serikali Bi. Ziada Sellah, amesema lengo la kukutana na wauguzi viongozi hao ni kuhakikisha wanafanya tathimini ya mwaka ya huduma za uuguzi na ukunga katika hospitali za rufaa za mikoa iliwaweze kufahamu mafanikio na changamoto zilizopo ili waweze kutafuta njia sahihi ya kuzitatua ili jamii iweze kupata huduma bora yenye staha na inayojali utu.

Kwa upande wao wauguzi na wakunga viongozi waliuoshiriki kikao wameonesha furaha yao kwa kushiriki wa kikao hicho huku wakiahidi kuwa kuyafanyia kazi yale yote watakayojifunza baadaya kujengewa uwezo.





# Mhe. Jenista Mhagama: Kurejeshwa Kwa Toto Afya Kadi Kutaleta Matumaini Mapya.

Na. Ezekiel Nyalusi

Waziri wa Afya Jenista Mhagama, amesema mabadiliko ya kurejeshwa kwa Toto Afya Kadi kutaleta matumaini mapya na uelekeo thabiti wa Bima ya Afya hususani kwa kundi la watoto ambalo linahitaji uangalizi wa pekee.

Mhe. Mhagama, ameyasema hayo 17, Disemba 2024 Jijini Dodoma, wakati akizindua vifurushi vitatu vya Bima ya Afya kikiwepo cha Toto Afya Kadi, amesema mpango huo wa Toto Afya Kadi utasaidia familia za wananchi hasa zile zenye watoto wenye changamoto za kiafya.

***"Mpango wa sasa wa usajili wa Toto Afya Kadi, utafanyika pia kwa mtoto mmoja mmoja iwapo itatokea mtoto husika hayupo shule, hii ni hatua kubwa na yakujivunia katika sekta nzima ya Afya.***

***mbali na kifurushi cha Toto Afya Kadi kilichozinduliwa leo, vifurushi vingine ni Ngorongoro chenye huduma 445 na Serengeti chenye huduma 1,815 ambavyo vyote vimelenga kuhudumia watanzania"*** Alisema Mhe. Waziri

Naye Mkurugenzi Mkuu wa NHIF Dkt. Irene Isaka, amesema kuzinduliwa kwa mfumo wa kidijitali




kumewawezesha kushughulikia folio 1200 kwa dakika 45 tofauti na awali ambapo walishighulikia folio 800 tu kwa siku.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima nchini Bw. Edga Gabriel amesema kuzinduliwa( kwa nini) kutasaidia kutambua viashiria vya awali vya udanganyifu, hivyo wanaipongeza NHIF kwa ubunifu huo.

Serikali kupitia NHIF imefanikiwa kutengeneza mifumo ya kidijitali kwa gharama ya Shilingi Bilioni 4.45 kwa kutumia wataalam wa ndani na kuokoa zaidi ya Shilingi Bilioni 3.5 endapo wangetumia wataalam kutoka nje ya nchi.



# Nchi 14 Zajifunza Kwa Tanzania Kupunguza Vifo Vya Mama Na Mtoto







**Na. Mwandishi wetu**

Serikali ya Tanzania imepokea ugeni wa wajumbe kutoka nchi 14 ukiongizwa na Shirika la kuthibiti magonjwa Afrika (CDC Afrika) kwa lengo la kujifunza namna Serikali ya Tanzania ilivyopiga hatua kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi na watoto wachanga.

Wajumbe hao wamefanya ziara katika kituo cha Afya cha Soya kilichopo Wilaya ya Chemba mkoani Dodoma Disemba 5, 2024 wakiongozwa na watendaji kutoka Wizara ya Afya Idara ya huduma za Afya ya uzazi, mama na Mtoto.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo Mkuu wa Progamu ya Uzazi Salama Wizara ya Afya Dkt. Phineas Sospeter, amesema Tanzania ni miongoni mwa nchi chache Barani Afrika zilizoweza kupunguza vifo vya wajawazito kwa kiasi kikubwa ambapo toka miaka saba iliyopita vifo vitokanavyo na uzazi vimepungua kutoka 556 kwa kila vizazi hai 100,000 kwa mwaka 2015/2016 na kufikia vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2022.

***"Hizi nchi kumi na nne zimekuja kujifunza namna tunavyotekeleza afua mbalimbali, wameweza kujifunza namna mifumo ya Afya inavyofanya kazi kutoka ngazi ya taifa hadi chini kwenye Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, na kuona namna utashi wa kisasa ulivyochangia kwa kiasi kikubwa katika kupunguza vifo hivyo,"*** amesema Dkt. Sospeter.

Naye Mganga mfawidhi kituo cha Afya cha Soya Dkt. Sabuni Kasongi, amesema jumla ya kinamama 83 wamepatiwa huduma za kujifungua kwa njia ya upasuaji wa dharura tangu kuanzishwa kwa huduma hiyo mwezi Oktoba 2023 katika kituo cha Afya cha Soya kilichopo Halmashauri ya wilaya ya Chemba.

***"Wajawazito na watoto wachanga wenye changamoto mbalimbali zinazowalazimu kupewa rufaa tunawapeleka hospitali ya wilaya ya Chemba na ya mkoa wa Dodoma kwa kutumia usafiri wa m-mama au ambulance, kwa upande wa wa m-mama jumla ya watoto waliofaidika na huduma hiyo ni 22 na wajawazito 72 tangu mfumo huo ulipoanza mwaka 2022,"*** ameeleza Dkt. Kasongi.

Wajumbe waliofika nchini kujifunza ni kutoka nchi ya Ethiopia, Gambia, Lesotho, Eswatini, DRC Congo, Chad, Nigeria, Somalia Guniea, Kenya, Uganda, Zambia, Misri na Sudan Kusini.

# Watahiniwa Mtihani wa Leseni Wasema Mafunzo kwa Vitendo Kujiamini ni Siri ya Kufaulu.

Ni mwandishi Wetu



Janeth Hamza-Mtahiniwa.

Baadhi ya watainiwa wa Mtihani wa usajili na Leseni kutoka kituo cha Chuo Kikuu Cha Kampala wameeleza kuwa, miongoni mwa siri muhimu za kufaulu mtihani wa usajili na leseni kwa watahiniwa wa ngazi zote ni kuzingatia mafunzo kwa vitendo wanapokuwa vyuoni, kuondoa hofu na kujiamini.

Wakizungumza na TNMC habari Disemba 19. 2024 siku moja kabla ya Mtihani katika viunga vya kituo hicho cha Chuo kikuu cha Kampala kilichopo Gongolamboto Jijini Dar es Salaam, watahiniwa Janeth Hamza, kutoka Chuo cha Afya Tanga, Crispin Christian, Chuo cha Afya Njombe na Daniel Masalu wa Chuo Kikuu cha Muhimbili, wamesema kwa upande wao wamejiandaa vema kuukabili mtihani huo kwa kuwa walipokuwa vyuoni walipata mafunzo ya kutosha kwa upande wa vitendo

***"Kumekuwa na fununu nyingi kuwa mtihani wa leseni ni mgumu na watu wanafeli, mimi binafsi naamini kuwa sio kila kinachokuwa kigumu kwa mwingine ni lazima kiwe kigumu kwangu pia, binafsi nipo tayari kuufanya mtihani na naamni nitafaulu kwa kuwa nimepata mafunzo ya kutosha ya vitendo nilipokuwa chuoni na chuo nilichosoma cha Tanga, kina hospitali ambayo ilituwezesha kuhudhuria mafunzo ya vitendo kwa usahihi katika Nyanja zote, lakini pia siri nyingine ni kujiamini ukijiamini kuwa ninaweza kilakitu kitawezeakana kwani mafanikio yanaanza kwa kujiamini"*** Alisema Janeth Hamza.



Daniel Masalu-Mtahiniwa.

***"Nipo yatari kwa Mtihani kwani wakati wa mwaka wangu mmoja wa mafunzo kwa vitendo niliweza kupata mafunzo kwa vitendo katika idara tofauti tofauti hivyo naamini nitaweza na huu matazamo kuwa mtihani utakuwa mgumu, mimi sina imani hiyo kwa sababu, tumeambiwa kuwa kinachoulizwa ni kilekile tulichojifunza kwenye vituo vyetu tulivyoapangiwa vya Internship".*** Aliongeza Daniel Masalu

Zaidi ya Watahiniwa 1,300 Wamefanya Mtihani wa Usajili na Leseni Ijumaa 20/12/2024 katika kituo cha Chuo Kikuu cha Kampala huku Jumla ya watahiniwa hao ikiwa ni 5147 walifanya katika vituo vilivyotengwa kwenye mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam, Iringa, Tabora, Mwanza na Arusha.

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania TMNC ni mamlaka ya kisheria inayosimamia wanataaluma na taaluma za uuguzi na ukunga Tanzania, Chini ya Sheria ya Uuguzi na ukunga ya mwaka 2010 na kanuni zake (The Nursing and Midwifery Act 2010) ili kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa na wauguzi na wakunga nchini zinakiwango kinachokubalika na salama kwa jamii.



# “Leseni Kwa Muuguzi, Mkunga ni Kibali Cha Utoaji Huduma” - Bi.Jane Mazigo

Na. Mwandishi wetu

***“Leseni ni utambulisho kwa muuguzi na mkunga kutoa huduma kwa jamii na ipo kwa mjibu wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010 hivyo, ni vyema kwa Muuguzi na Mkunga kuwa na leseni iliyo hai muda wote wa kutoa huduma”.***




Hayo ameyasema Bi.Jane Mazigo, Mkurugenzi wa Maadili, Usajili na Leseni akizungumza na TNMC Habari Bi. Mazigo, ameongeza kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga kifungu cha 21 (A) na (B) Sheria inafafanua majukumu ya msajili wa TNMC kuwa ni kumsajili Muuguzi na Mkunga na kumpa leseni pamoja na kuhuisha leseni hiyo mara inapokwisha muda wake kwa mujimu wa miongo ya Baraza.

*"pia kwa mujibu wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga kifungu cha 38 inaeleza adhabu ambazo muuguzi na mkunga atakumbana nazo pindi atakapobainika akitoa huduma pasipo kuwa na leseni hai”* alisema Bi.Mazigo

Katika hatua nyingine Bi.Mazigo, amewakumbusha waajiri wa wauguzi na wakunga kote nchini, kuhakikisha wanazingatia leseni kwa wataaluma hao kabla ya kuwaajiri kwani ni kosa kisheria kwa mwajiri kumwajiri na mtoa huduma za Uuguzi na Ukunga pasipokuwa na leseni na utaratibu huu ni wa kimataifa na unalengo la kulinda Afya ya Jamii zinazopokea huduma duniani kote.

Zaidi ya wauguzi 6,000 wanatakiwa kuhuisha leseni zao katika kipindi cha kuanzia tarehe 01 Julai mpaka 30 Disemba 2024 kwa gharama za kawaida na baada ya muda huo kupita mfumo utaanza kutoza pamoja na penati.






# Tanzia

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania limepokea kwa Masikitiko vifo vya wauguzi na wakunga wenzetu waliotangulia mbele ya haki Mwezi Disemba, 2024, baada ya kumaliza kazi ya hapa Duniani, Mwenyezi Mungu azilaze Roho zao Mahali pema Peponi AMENI.



JINA: Sr Anatolia Felix Chuwa
KITUO: Zahanati ya James Nevile
WILAYA: Moshi
MKOA: Kilimanjaro



JINA: Teresia John
KITUO: Hospitali ya Maswa
WILAYA: Maswa
MKOA: Simiyu



JINA: Bonitus Rwetambula
KITUO: kituo Cha Afya Ujiji
MANISPAA: Kigoma Ujiji
MKOA: Kigoma



JINA: Agness Sylvester
KITUO: hospitali ya Oltrumet
MKOA: Arusha



JINA: Martha Tumaini Mshashi
MKOA: Morogoro

JARIDA LA BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA

Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano
Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania
S.L.P 1736 DODOMA , **Simu: 0736 00 60 60**
Barua Pepe:Info@tnmc.go.tz
Tovuti:www.tnmc.go.tz

HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA